



>>LINAUNGANISHA kata tatu za Rungwe >>Mwananchi apasua mazito yaliyokuwepo



Daraja Landani - Masukulu, alama ya furaha kwa maelfu ya -wananchi

Na **CHARLES MGANGA**, RUNGWE

DARAJA miundombinu muhimu kwani ni kiunganishi kutoka upande mmoja hadi mwingine kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao.

Sehemu linapohitajika daraja pindi likakosekana, wananchi huwa katika wakati mgumu pindi inapotokea changamoto upande mmoja kuhitaji kwenda ng'ambo kwa ajili ya mahitaji au hudumu za msingi.

Changamoto kubwa hasa huwa ni usafiri na zaidi waathirika wakubwa huwa akinamama wajawazito, wagonjwa na hata wanafunzi wanahitaji kwenda shule kama iko upande mwingine kwa ajili ya kupata elimu.

Lakini kwa kuona umuhimu wa miundombinu hiyo serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli, pamoja na mambo mengine, ilijenga madaraja katika maeneo tofauti.

Kufanya hivyo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 hadi 2020.

Katika kipindi cha miaka mitano, miradi kemkem ya maendeleo imetekezwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja ambayo yamewasaidia wananchi kufanya shughuli zao za ujenzi wa taifa na zile za kujitafutia kipato bila wasiwasi tofauti na ilivyokuwa zamani.

Daraja la Landani kwenda Isabula hadi Masukulu ni moja kati ya mradi wa ujenzi wa kuondoa vikwazo katika barabara za vijijini (Bottle-neck) chini ya ufadhili wa serikali ya Uingereza.

Kwa mujibu wa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri ya Rungwe na ile ya ujenzi wa daraja hiyo kwa kiongozi wa mbio za mwenge mwaka juzi, Charles Kabeho, utekelezaji wake ni juhudi za serikali ya awamu ya tano katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja vijijini.

Taarifa ya ujenzi wa daraja hiyo inaeleza kuwa shughuli zilianza kutekezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na ukamilika Juni mwaka juzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter,

anasema madaraja mawili yamejengwa ambapo kila moja limegharimu sh. bilioni 1.08.

Madaraja hayo ya Landani kwenda Masukulu na lile lililopo Kisondele, yanaunganisha kata kadhaa.

"Tulianza na ujenzi wa daraja kwanza kabla ya barabara inayounganisha kwenda Busokelo nyingine inakuja kwenye kata hizo.

"Wananchi wamerahisishiwa sana kusafirisha mazao yao kwenda soko na sasa nafikiri wanafurahia maisha," anasema mkurugenzi Loema.

MWANANCHI WA ISABULA

Rafael Mwamwaja ambaye ni mkazi wa kitongoji cha Isabula, sehemu ambayo ni jirani na daraja la Mwalisi anasema daraja hilo limewaondolea adha waliyokuwa wakiiipata kabla halijajengwa.

Anasema kabla halijajengwa daraja hilo linalounganisha kata za Matwebe na Masukulu, walikuwa wakiwabeba wagonjwa migongoni kuwapeleka hospitali kutokana na kutokuwepo miundombinu hiyo.

"Tulikuwa tunawabeba wagonjwa mgongoni au kwa machela kuwapeleka katika kituo cha afya Masukulu, wapo wengine walipotewa maisha kutokana na adha hiyo ya kukosa daraja.

"Tunaishukuru serikali imetusaidia sana. Hivi sasa hatuna shida kabisa, wagonjwa tunawapeleka hospitali kwa kutumia usafiri wa magari au bodaboda.

"Kipindi cha mafuriko tulikuwa tunawabeba wagonjwa, tunaanguka kwenye maji. Lakini, hivi sasa tunafurahi tunaweza kulitumia daraja nyakati zote.

"Tunakishukuru Chama Cha Mapinduzi ambacho ndicho chenye serikali kwa kuona kuna umuhimu wa sisi kujengewe daraja hili.

"Kwa hakika shukrani zetu ziwafikie wote kwa uamuzi wao wa kutuungalia kwa huruma," anasema mkazi huyo wa Iseselo.

BARABARA ZA LAMI

Kuhusu ujenzi wa barabara za lami, mkurugenzi wa halmashauri ya Rungwe, anasema unaendelea katika maeneo tofauti.

Anaeleza kuwa hivi sasa zinajengwa kuelekea Chuo cha Mpuguso.

"Tunaendelea na ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami, kwa sasa kazi inaendelea zikiwemo zile ambazo zimeshajengwa katika kipindi cha miaka mitano hii ya awamu ya tano," anasema mkurugenzi.

MIRADI YA MAJI

Anasema kuna miradi mikubwa miwili ambayo ikikamilika ujenzi wake, upatikanaji wa maji vijijini utafikia asilimia 85.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, wao wana bahati kuwa na maji mengi kupitia chanzo cha mlima Rungwe, lakini miundombinu ya kuvuta maji kwenda kwa wananchi inaendelea kufanyika kupitia fedha zinazopatikana.

Miradi mikubwa inayotajwa ni Masoko group' ambao uko asilimia 90 na 'Mwakaleli group,' awali ilikuwa na changamoto, lakini zimetatuliwa.

"Hii ni miradi ya muda mrefu sana, ilikuwa na changamoto ambazo tumezitatua kabla ya kwenda RUWASA, sasa hivi wanajenga kwa 'Force Account' hasa wa Masoko group ambao umebaki kipande kimoja kukamilika.

"Mradi huu unanufaisha vijiji zaidi ya 15. Ule wa Mwakaleli, ukikamilika upatikanaji wa maji utafika asilimia 85 kama nilivyosema," anasema Loema.

UWEZESHAJI KIUCHUMI

Anasema halmashauri ya Rungwe katika mwaka wa fedha 2015/2016, mikopo iliyotolewa kwa wananchi ilikuwa sh. milioni mbili tu ukilinganisha na sasa ambapo kiasi cha zaidi ya sh. bilioni moja.

Mkurugenzi mtendaji anasema tayari wanufaika 3,500 ambao wako katika vikundi tofauti, wameshapata mikopo.

"Hao wameshaimarisha hali zao za kiuchumi tayari, Septemba 21, mwaka huu nitatoa mikopo wa sh. milioni 152 kwa vikundi 21 ambapo ndani yake wanufaika ni wengi," anasema mkurugenzi mtendaji wa Rungwe.

Jumla ya wakazi 4551 wamenufaika ikiwa ni vikundi 135 kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020.

MAPATO YA NDANI

Utegemezi wa mapato ya ndani, umeendelea kuimarika kutokana na makisio ya mapato ya ndani kuongezeka.

Anasema wakati serikali ya awamu ya

tano ilipoingia madarakani, halmashauri ya Rungwe ilikuwa ikiweza kujitegemea kwa mapato ya ndani kwa asilimia sita tu.

Mkurugenzi anasema mpaka sasa utegemezi wa halmashauri hiyo umeimarika kutoka asilimia 6 hadi 11 kutokana na kuimarisha mapato ya ndani.

"Mwanzo asilimia 94 ya mapato, ilikuwa ikitegemea kutoka serikali kuu. Sasa tumepandisha mpaka asilimia 11, hii ni kutokana na kuongeza uwezo wa halmashauri kujitegemea na kupandisha makisio ya bajeti na ukusanyaji mapato," anasema.

Kuongezeka huko, kunafanya baadhi ya mambo kufanyika kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani.

MAENEO YA BIASHARA

Kuhusu maboresho ya maeneo ya kufanyia biashara, mkurugenzi mtendaji Loema, anasema wameweka mazingira rafiki katika soko la Tukuyu Mjini baada ya kuwepo mahitaji makubwa.

Anasema eneo hilo limejengwa vibanda vingi vya kufanyia biashara, halmashauri inaendelea kuboresha masoko ya Tandale, Mpuguso na Kiwira.

Anasema pia soko jipya la Mwambenja, linatarajiwa kujengwa, lengo ni kuwasogezea huduma wananchi huku halmashauri ikishirikiana nao kuanzia hatua za awali.

TUKUYU BUSSINESS CENTRE

Anasema litajengwa jengo hilo baada ya kuendelea kubaini bado kuna mahitaji makubwa ya wafanyabiashara kufanya shughuli zao.

"Pamoja na ujenzi wa masoko hayo katika maeneo mbalimbali, tuliona upo umuhimu wa kujenga jengo la ghorofa ili kutumika na wafanyabiashara wengi kwa sababu halmashauri yetu ardhi yetu si kubwa," anaeleza.

VITAMBULISHO WAJASIRIAMALI

Mkurugenzi mtendaji huyo anasema utaratibu wa kugawa vitambulisho kwa maelekezo ya Rais Magufuli, unafanyika ili wasisumbuliwe na wenye dhamana ya kukusanya kodi.

Anasema mwaka jana, halmashauri ilitoa kwa asilimia mia moja kutokana na mgawo wao, hali hiyo itaendelea hivyo.

Mkurugenzi huyo anaeleza kuna changamoto kadhaa kwa wanaopewa vitambulisho hivyo wakiadini hawatakiwi kulipa hata kodi ya pangam.

"Awali, hawakuelewa kutokana na mfumo mpya wa biashara, lakini tuliwaelimisha na wafanyabiashara wengi hivi sasa wanaelewa," anaeleza.

VIVUTIO VYA UTALII

Loema anasema halmashauri ya Rungwe imebarikiwa na hali ya hewa nzuri na vivutio vya aina tofauti.

"Niseme tu kuwa Rungwe ndiyo inabeba mkoa wa Mbeya kwa wingi wa vivutio. Lakini, changamoto hapa hatujavitangaza sana.

"Vivutio hivi ni kati ya vyanzo vya mapato, licha ya kwamba hatujafanikiwa sana kukusanya mapato," anasema.

Anasema moja kati ya changamoto ni miundombinu ya barabara na vyoo katika maeneo vilipo vivutio, ingawa halmashauri imeendelea kuvitatu.

Anasema katika kivutio cha Daraja la Mungu, halmashauri inakusanya mapato, ingawa si kwa kiwango kikubwa kutokana na watalii kutoelewa eneo hilo.